ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi – Tarehe 12 April, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumwita Mhe. Hija Hassan Hija atuwasilishie hati, naomba kutoa taarifa ya wageni wetu waliopo katika eneo la wageni wa Spika pale juu ambao wageni wenyewe ni kama ifuatavyo:

Leo tarehe 12/04/2012 katika ukumbi wetu wa juu wa wageni wapo wageni na wanafunzi wa Skuli ya Potoa iliyopo Mkoa wa Kaskazini, wanafunzi hao wanaongozwa na Mwalimu Mkuu ndugu Hamad Abuu Hamad na Mtumwa Mjomba pamoja na Rais wa Wanafunzi ndugu Khamis A. Mdungi. Tunaomba Waheshimiwa Wajumbe tuwatambue wageni wetu hao na kuwaomba wageni wenyewe pia nao wasimame ili muwaone. Karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi na Rais wa wanafunzi ili kuona shughuli za Baraza hili ambalo ni Baraza lenu wananchi, nakushukuruni sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani taarifa ya hoja binafsi kuhusu Kuunda Kamati Teule ya Kuchunguza Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) dhidi ya madai ya kuwepo ukiukwaji mkubwa wa majukumu yake. Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 107

Wafugwa Kupewa Mlo Mmoja Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ripoti ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2007/2008 hapa Zanzibar imebainisha kuwa wafungwa (Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo) wamekuwa wakipewa mlo mmoja badala ya mitatu kwa siku.

a) Mhe. Waziri sababu gani inepelekea wanafunzi hao kupewa mlo mmoja kwa siku wakati kitendo hicho ni kinyume na misingi ya haki za binadamu.

b) Mhe. Waziri je, sababu gani zinazopelekea wafungwa kutokupewa nyama, samaki na matunda bila kuzingatia kazi ngumu wanazofanya.

c) Serikali katika mwaka wa fedha 2011/2012 imepanga kutumia bajeti ya chakula kiasi gani katika mwaka wa fedha 2011/2012.

d) Je, serikali ina mpango gani wa kuondoa vyoo vya ndoo katika magereza yetu kama ilivyoamuliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 107 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kimeanzisha utaratibu wa kulisha wanafunzi walioko vyuoni milo mitatu kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

b) Serikali kupitia vyuo vya mafunzo vinajitahidi kuhakikisha kwamba wanafunzi waliomo ndani ya vyuo hivyo wanapata chakula kilichobora. Katika baadhi ya siku wanafunzi hao hupewa nyama na samaki hususan katika siku za sikukuu mbali mbali.

c) Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 400,480,000/= kwa bajeti ya chakula kwa wanafunzi wa Vyuo vya Mafunzo.

d) Mhe. Spika, serikali tayari imeshakamilisha ujenzi wa vyoo vya kutimia sinki katika Vyuo vya Mafunzo vya Kangagani na Tungamaa kwa upande wa Pemba na Langoni na Kinumoshi kwa upande wa Unguja. Aidha, sehemu ya wanawake katika Chuo cha Mafunzo cha Kiunua miguu nayo pia imejengewa vyoo vya aina hiyo.

Mhe. Spika, kazi ya kuendeleza ujenzi wa vyoo katika vyuo vilivyobaki inaendelea vizuri, kiasi ya kuridhisha tume ya haki za binadamu na utawala bora. Naomba Mhe. Spika, nitamke kwamba kwa kweli hii Tume ya Haki za Binadamu imekuwa inatembelea mara kwa mara Vyuo vya Mafunzo na niseme kwamba vyuo vyetu vya Zanzibar tumepata sifa kwa kutimiza zile haki za binadamu kwa wanafunzi wetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa lishe ni jambo muhimu kwa binadamu, kanuni za lishe bora zinasema kuhusu matumizi ya vyakula ikiwa nyama, mboga mboga, samaki.

a) Je, wanafunzi hao itabidi wasubiri sikukuu hadi sikuku ndio wale chakula hicho.

b) Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa mwaka huu kuwalisha wanafunzi mara tatu kwa siku ambapo hapo nyuma ilikuwa ni mara mbili, hilo nikupongeze Mhe. Waziri kwa jitihada ulizozifanya. Lakini Mhe. Waziri kutokana na bajeti unayowapa kwa chakula unajua kuwa haikidhi kabisa na hivi sasa kumekuwa na deni karibu milioni 26 za nguo mpya wanazovaa hivi sasa watu hao wa magereza. Je, una mpango gani wa kukisaidia chuo kile katika bajeti inayokuja ili kuwaondoshea mzigo mzito pamoja na kazi nzito wanazozifanya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba lishe bora ni suala la msingi kwa binadamu yeyote hasa kwa hawa wanafunzi ambao wamefanya makosa na niseme kwa bahati mbaya wako kizuizini kule wanafundishwa kuwa raia bora. Kwa kweli nakubaliana pia kwamba bajeti iliyopo haitoshi, sasa kwa kuwa mantiki hiyo katika vyuo vyetu vyote vya mafunzo vilivyoko nje ya mji tumeanzisha utaratibu wa kilimo cha mboga mboga kwa hawa wanafunzi wetu. Ni kwamba wanalima mboga mboga, wanafuga kwa kujisaidia kwa kitoe na matumizi ya chakula.

Mhe. Spika, kwa kweli sote tunakubali na Mhe. Mwakilishi na yeye anakubali siku hizi matunda yamekuwa ghali kuliko ule mlo wenyewe, labda utuhamasishe tupate embe za Muyuni ili tuwasaidie wanafunzi, na boribo za Muyuni ni nzuri sana kwa hiyo utuhamasishe ili tuzalishe kwa wingi halafu sisi tuko tayari kununua kwa kuwasaidia wanafunzi. Lakini nakubaliana na wewe kwamba bajeti ni ndogo lakini tunajitahidi wenyewe kulima ili kusaidia kupunguza hali ya bajeti.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyoongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, nilipata habari kwamba wizara ina mpango wa kujenga chuo kipya cha mafunzo kitakachohimili na kufuata utaratibu wote wa haki za binadamu. Je, utaratibu huo bado upo na kama upo utajengwa pahala gani.

b) Mhe. Spika, mwaka jana nilisikia kwamba kuna mfungwa mmoja Bara alipata *degree* wakati yumo ndani ya Chuo cha Mafunzo. Je, suala la taaluma kwa vyuo vyetu vya mafunzo Zanzibar limezingatiwa vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kujenga Makao Makuu mapya ya Chuo cha Mafunzo kule Hanyengwa mchana, hapa Kilimani tayari pamekuwa padogo na *site* tayari tumeshakabidhiwa, imeshapimwa na michoro iko tayari sasa kadri pesa tutakavyopata tunatafuta *contractor* ili tuanze ujenzi mara moja. Mhe. Spika, jengo hilo

litakuwa ni la kisasa na tumefuata mashauri au maelekezo mengi sana ya haki za binadamu katika gereza au katika chuo kile hasa kutenganisha wanafunzi na watu wazima, na wanawake pamoja na wanaume.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba hivi karibuni alifariki mwanafunzi mmoja kwa maradhi ya *TB*, hiyo ni kweli na yeye alikuwa ni mgonjwa kama wa siku nyingi, na hii imetokezea bahati mbaya kwamba yeye yuko kizuizini ndio imetokezea, lakini maradhi ya *TB* yanatokezea pahala pengine popote. Lakini tuna utaratibu mzuri wa kufukizwa kule chuoni mara kwa mara na tunashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Afya kwa kutusaidia kufukiza kule na pia hata wanafunzi wale huwa wanatizamwa mara kwa mara na madaktari.

TAARIFA

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, mimi nimemuuliza swali jengine Mhe. Waziri amejibu vyengine ambavyo sikumuuliza. Mimi nimeuliza wenzetu Tanzania Bara gereza la Ukonga mwaka jana mwanafunzi alipata *degree* kwa kujiendeleza wakati yumo ndani ya kazi za ufungwa. Je, katika magereza yetu ya huku Unguja suala la taaluma tumelipa nafasi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kumradhi kidogo nilisikia *TB* kumbe ni *degree*, samahani Mhe. Mwakilishi sikulisikia vizuri hilo suala.

Mhe. Spika, mpango huo na sisi tunao wakuwafunza wanafunzi wetu na zaidi tunawafunza mafunzo ya amali, tayari kule wako ambao wanaochonga, wako ambao wanashona. Lakini hatujafika kwenye masomo ya nadharia kama vile *degree*, kwa hiyo ushauri wake tunauchukua na tutakwenda kusoma kwa wenzetu wanatumia utaratibu gani ili tuwaendeleze kwa taaluma wanafunzi wetu.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, hivi juzi tu kabla ya sherehe ya Pasaka nilifanya ziara ya ghafla moja ndani ya magereza yetu ya Zanzibar eneo lile la mafunzo, kwa bahati mbaya nilifika pale kuonana na maafisa wakanielezea jinsi gani wanavyopata tabu katika kupambana na shida ya maji ambayo inapelekea hata yale maji ya kunawia uso asubuhi wakawa hawana. Lakini kama hilo halitoshi na wanasumbuliwa wanapoumwa na vichwa hata ile *panadol* ndani inakuwa hamna.

Je, Mhe. Waziri utalieleza nini Baraza hili tukufu kuhusu suala hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni na Chuo chetu cha Mafunzo kiko katika eneo lake kwa kupita na kutukagua na kuweza kubaini baadhi ya matatizo. Kwa hivyo, namuomba awe karibu zaidi ili tuweze kufanya kazi zaidi hasa hili suala la maji.

Mhe. Spika, ni kweli kuna matatizo ya mtandao wa maji, lakini pale tumechimba kisima na hicho kisima ndicho kinachookoa jahazi katika Makao Makuu ya Chuo cha Mafunzo pale Kilimani.

Mhe. Spika, kuhusu dawa nafikiri wiki iliyopita nilizungumza labda bahati mbaya hukuwepo, lakini kweli tumetenga fedha kiasi kwa ununuzi wa dawa katika hospitali yetu pale na hospitali ile inatumika kwa wanafunzi wenyewe na hata kwa watu wa nje.

Mhe. Spika, pia tukasema kwamba tunamashirikiano mazuri na *NGO* iliyopo Dar es Salaam ina *Pharmacy* wanatusaidia hasa dawa za ukimwi na dawa nyengine, na pia katika matibabu mazima ya wanafunzi.

Kwa hivyo, nakiri kwamba kuna mapungufu lakini tunajitahidi kwa bajeti yetu na kushirikiana na washirika wengine wa maendeleo kusaidia upatikanaji wa dawa kwa wanafunzi wetu.

Nam. 108

Samaki Kukatwa na Kuuzwa Chini ya Barabara Sokoni Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

a) Mhe. Waziri kwa vile Soko la Darajani ni moja ya kivutio cha watalii kwa nini samaki wanaendelea kuuzwa chini kwenye barabara katika soko hilo.

b) Je, wizara yako inachukua hatua gani ya kuzuia samaki kuuzwa chini kwenye soko la Darajani.

c) Hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji wa soko hilo ambao wameshindwa kusimamia kanuni za usafi maeneo yao ya kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 108 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Mwakilishi kwamba kanuni za afya haziruhusu bidhaa za chakula kama vile samaki na nyenginezo kuuzwa chini ya barabara hasa pembezoni mwa barabara. Katika soko la Darajani biashara ya kuuza samaki chini huwa zinafanywa nyakati za jioni ukienda sasa hivi hawapo watu wale huwa wanaanza jioni wakati soko limefungwa mpaka Magharibi, na biashara hizo huwa zinafanywa na wafanyabiashara wadogo wadogo. Mhe. Spika, kufanya hivi ni kinyume na taratibu zilizowekwa na Baraza la Manispaa Zanzibar.

b) Mhe. Spika, napenda kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Manispaa inachukua juhudi za kuwaondoa wafanyabiashara hao kwa kufanya *operation* mara kwa mara na wanaokamatwa huwa wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria. Baraza la Manispaa pia inachukua hatua za kuwaondoa wafanyabiashara hao zaidi kwa njia za busara badala ya kutumia nguvu kwa kuepusha malumbano. Hatua hizo ni pamoja na kuelimisha wafanyabiashara hao kwa kushirikiana na umoja wa wauza samaki wa soko la Darajani. Naomba Mhe. Mwakilishi na yeye kwa upande wake atusaidie kwa wananchi wale wanaouza pale najua wengi ni rafiki zake kidogo.

c) Mhe. Spika, hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi wa Baraza la Manispaa wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao zinachuliwa ikiwa ni pamoja na kuwapa onyo na kuwabadilisha sehemu zao za kazi. Hata hivyo, Mhe. Spika, kutekeleza na kusimamia usafi ni jukumu letu sote kama wakaazi wa Mji wa Zanzibar, sio jukumu la Baraza la Manispaa peke yake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kilichonitia moyo zaidi ulivyotumia neno busara kwa kuwaelimisha watu wale nimefurahi sana Mhe. Waziri kwa hilo. Lakini je, huoni hii biashara wanaoifanya jioni kutokana na dhiki ya wananchi kuwa wanashinda ya maisha walioyokuwa nayo, huoni kama wana haki katika serikali hii wananchi wale wakatafutia eneo ili wakaelimishwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ushauri wake ni mzuri tunaukubali inafaa watu wale tuwapatie sehemu waweze kujisaidia kupata mapato na kuendesha maisha yao. Lakini kama nilivyosema zaidi pale wanakuwa jioni na sio wauza samaki tu, hata wengine wanauza mboga mboga, wengine mashelisheli, wengine maziwa hivyo inakuwa haipendezi kwa hiyo naomba tusaidiane sote ili tuweze kuwaelimisha watu wale na sisi serikali tutajitahidi kwa upande wetu kuwaweka mahala muafaka.

Mhe. Nassor Ali Salim: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali na samaki wale wanaouzwa pale Darajani chini, lakini kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara wa samaki kuuza samaki katika maeneo ya Mnazi Mmoja karibu na nyumba ya Makamo wa Rais.

Je, wizara haioni kwamba kuuzwa samaki pale ni kumpa harufu mbovu Makamo wa Rais wa Zanzibar.

Mhe. Spika: Mheshimiwa suala lilikuwa linahusu soko la samaki la Darajani, lakini labda tumsaidie kidogo lakini pale sio sehemu ya soko la Darajani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Ni kweli na sio pale Mnazi Mmoja tu, lakini siku hizi sehemu nyingi za njiani unajua wafanyabiashara wana mbinu za biashara na wanaona Mhe. Mwakilishi ukipita na gari lako pana samaki mzuri pale wa changu, tasi na mwengineo utasimama. Lakini utaona tabu kwenda ku-*park* gari yako ukenda kwenye soko, hilo ndio tatizo madereva ndio sisi na tunaonunua ni sisi, lakini kama tutaacha tabia ile ya kununua basi wataondoka wale. Mhe. Spika, mimi naweza kusema ni sisi wenyewe tuwaekee mgomo baridi tusinunue mle njiani basi wengi wao watahama, lakini ikiwa tunanunua basi tunawapa soko. Kwa hivyo, nakubaliana na yeye kama pale sio pazuri na mara nyingi

kama nilivyosema huwa tunajitahidi kuwaondoa na gari letu la Manispaa mara nyingi utawaona vijana wanafanyakazi. Lakini ndio yale niliyosema kwamba tutoe elimu kwa vijana hawa ili mle ambamo hamfanyi biashara basi wasifanye.

Mhe. Ali Abdall Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na kuondosha kero la wauza samaki nje lakini pia kuna tatizo la matumbo ya samaki yanakaa muda mrefu kwenye kontena na kuleta harufu mbaya. Je, na hili wizara italifanyia utaratibu gani ili Mji wetu uwe na haiba nzuri..

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba yale matumbo ya samaki huwa yanaleta bughudha katika majaa yale. Lakini kiutaratibu yale matumbo ya samaki huwa yanawekwa sehemu maalum hayapaswi kuchanganywa na taka. Kwa hivyo, kama yanachanganywa na taka huwa ni bahati mbaya, ndio hao wafanyabiashara wengine wadogo wadogo wasiojua zile taratibu. Lakini pale Marikiti yale huchukuliwa yakawekwa sehemu maalum, na tunatoa vipaumbele kwa taka zile za matumbo ya samaki na nyenginezo kama zile kuondolewa Mjini haraka sana. Hivyo tutajitahidi kuona kwamba suala hili tunalishughulikia ipasavyo.

Nam. 32

Hospitali ya Chake Chake

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Hospitali ya Chake-Chake katika eneo la kujifungulia hakuna stara. Hata mtu asiyehusika anaweza kupita na akaona shughuli zote za uzalishaji jinsi zinavyoendelea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha sehemu ya kujifungulia ili iwe stara na iweze kumpa uhuru mama mjamzito ajifungue kwa salama na faragha.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake katika wodi ya kuzalia ulijumuisha wodi mbili, moja ya kabla na ya pili baada ya kujifungua. Pia kuna chumba cha kuzalia ambacho imetengwa kidogo na wodi nilizozitaja hapo awali kwa madhumuni ya kuwapa utulivu akina mama ili weweze kupima maendeleo ya uchungu na hatimae kujifungua.

Mhe. Spika, jana nilieleza kwa urefu suala la ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake na Mhe. Mwakilishi linafanana na lile la jana hii sehemu ya pili. Kwa hivyo, ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake utategemea ule mpango wa wizara wa kuitengeneza yote nzima ikiwemo kufanya marekebisho makubwa katika sehemu ile.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, *concern* yangu hasa ilikuwa si ujenzi katika suala langu lile la mwanzo ndio kama nilivyosema suala hili liondoshwe na baadae ilikuwa kina mama zile *movement* za pale ndani zinakuwa hazina mpangilio inabidi inaleta usumbufu wanaingia watu ambao hawahusiki na hili ni ushahidi mimi mwenyewe binafsi juzi nilikwenda nikaona.

Mhe. Spika, kwa kuwa sehemu ya kujifungulia wazazi ni sehemu muhimu sana, na katika kuingia yangu pale sehemu ya kuzalia nilikuta vitanda vya kujifungulia wazazi ni vibovu, pia imekosekana *incubator* ya kuhifadhia watoto ambao wanazaliwa chini ya umri wa miezi 9.

Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wakuwapatia vifaa hivi muhimu ili ipatikane huduma bora ya mama na mtoto.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwama Mhe. Panya amefika pale na kuona hali halisi, mwanzo nilipokuwa najibu swali hili nilikuwa najiuliza huyu aliyefika kule akaona kwamba stara ni nani, kwa sababu mahala pale ni pa shughuli maalum na panaingia watu maalum kwa kazi maalum, sasa mwanzo nilicheka nikajiuliza huyu nani aliyefika huko kwenye stara kumbe ilikuwa ni mtu anayehusika na mambo ya kinamama. Nashukuru kwa hilo.

Kuhusu hivi vifaa tunavishughulikia na ni moja katika matatizo ya vifaa kwa hospitali nyingi tulizonazo hasa sehemu za uzazi, imo katika mpango mzima wa kushughulikia masuala ya *maternity* moja katika suala linalotusumbua ni vifaa vya uzazi. Kwa hivyo, namuahidi kwamba nitalifuatilia na kuona tunachukua hatua za haraka hasa kwa Hospitali ya Chake Chake pamoja na *incubator*.

Samahani Mhe. Spika, ninachokumbuka *incubator* zimo, kulikuwa na tatizo fulani kwamba wale wanaohusika kuzitumia hawafahamu jinsi ya kuzitumia *incubator* hizo na zimekuwepo siku nyingi sana, muda mrefu tumekuwa tunabishana baina ya kuwepo *incubator* na jinsi ya kuzitumia. Lakini nitalifuatilia Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kuna matatizo katika kituo hicho cha kujifungulia na kwa kuwa kuna sehemu moja tu ya kujifungulia. Je, atatuthibitishia Mhe. Waziri katika hiyo ramani yao ya ujenzi imo kuongeza kituo kipya cha kujifungulia pamoja na kuweka sehemu ndogo ndogo ambazo zitaweza kujifungulia mtu zaidi ya mmoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kuna mpango kamili wa vituo 34 zikiwemo Hospitali hizo za Chake Chake, Wete na Mkoani kuimarishwa sehemu za wazazi, vituo 34 Unguja na Pemba. Kama nilivyoeleza jana mafanikio ya mfano wa Makunduchi ndio tunaotaka kuutumia na kwa hospitali nyengine. Kwa hivyo, yale aliyoyashauri ndio tutakayoyatekeleza ili kutoa nafasi kimamama wasisumbuke, kama vituo vyote 34 Unguja na Pemba vitatoa huduma ya uzazi kama tunavyotegemea hakutakuwa na tatizo la mrundikano wa huduma hizo katika Hospitali ya Wete, Chake Chake na Mkoani au hospitali nyengine zote. Kwa hivyo, imo kwenye utaratibu wa matengenezo haya.

Nam. 35

Mapambano ya Malaria

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Pamoja na mafanikio ya jitihada za kupambana na malaria, inaonekana bado kuna dalili za kuibuka kwa kazi kwa malaria katika baadhi ya maeneo.

(a) Ni maeneo gani yaliyogunduliwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa Malaria.
(b) Je, hali hiyo mpya imechangia kuwepo kwa Malaria kwa kiwango gani.
(c) Je, dawa gani zinatumika kutibu malaria kwa uhakika katika maeneo hayo.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 35 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli kwa mujibu wa takwimu zinazokusanywa na Kitendo cha Malaria kuna maeneo ambayo yalionekana kuwa idadi ya wagonjwa waliougua malaria ilikuwa ikiongezeka ingawa si kwa kasi kubwa na Wizara ya Afya ilitoa taarifa kuhusu ongezeko hilo la ugonjwa wa malaria visiwani Unguja na Pemba kwenye baadhi ya maeneo kupitia kwenye vyombo vya habari.

(a) Maeneo ambayo yaligunduliwa kuwa na ongezeko la wagonjwa wa malaria ni kama yafuatayo:-

    (i) Wilaya ya Micheweni – katika vijiji vya Tumbe, Msuka, Makangale, Konde, Kinyasini, Shumba viamboni, Kiuyu Kipangani, na Mkia wa ng'ombe.
    (ii) Wilaya ya Chake Chake - katika vijiji vya Ziwani, Mkoani, Wambaa.
    (iii) Wilaya ya Wete - katika vijiji vya Junguni na Ukunjwi
    (iv) Wilaya ya Kaskazini B – katika vijiji vya Donge Mchangani, Donge Vijibweni, Misufini, Bumbwini na Zingwe Zingwe.
    (v) Wilaya ya Kati - katika vijiji vya Jendele, Uzini na Mchangani

(b) Kiwango cha ongezeko la ugonjwa wa malaria iliripotiwa katika wiki ya 47 ya mwaka 2011.

    Wastani wa wagonjwa wanne (4) waliripotiwa wiki ya 46 ya mwaka 2011.
    Wastani wa wagonjwa 17 hadi 63 waliripotiwa kwa wiki ya 47 ya mwaka 2011 hadi wiki ya 5 ya mwezi wa Februari, 2012.

(c) Dawa ambazo zimetumika kutibu malaria katika maeneo hayo ni dawa mchanganyiko ya Artesunate na Amodiaqune, ambazo ndizo zilizopendekezwa kutumika katika visiwa hivi.

Mhe. Spika, baada ya taarifa hii katika mfumo wetu wa kutibu malaria imekuwa kama ni vita, tukijua kwamba humu mna wagonjwa wataalamu wetu huenda moja kwa moja katika maeneo hayo na kupiga dawa na kutoa vyandarua kwa wakati maalum na kwa sababu maalum na kuhakikisha kwamba hawaondoki kwenye eneo hilo mpaka wawe wamehakikisha suala limemalizika. Kwa hivyo, kunakuwa na *surveillance* ya muda wote.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa majibu mazuri nay a kina ya Mhe. Waziri, lakini napenda nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Katika swali langu (b) nilitaka kujua Kizanzibar huku kuongezeka kwa malaria ile asilimia ngapi sasa imeongezeka kutoka ngapi kuja ngapi baada ya kutokezea ongezeko hili.

(b) Wananchi wengi wanababaishwa kidogo na hali inayojitokeza katika vituo vya kupima malaria. Wengi wanaokwenda wanaambiwa hawana malaria lakini baadae wanapewa dawa. Sasa je, haya ni maelekezo kutoka Wizara ya Afya kwamba wasiambiwe wana malaria lakini wapewe dawa? Ikiwa ni hivyo, hiyo *prevalence* itajulikana kwa kiwango gani ikiwa vile vituo haviripoti kwamba wagonjwa kadhaa wamepatikana na malaria na huwa wanaipata vipi, na wagonjwa wengi wanaambiwa hawana malaria vidudu havikuonekana na kumbe wanapewa dawa. Lakini vile vile mashine je zinazotumika sasa hivi zimepitwa na wakati kuwa wadudu hao waliojitokeza sasa hawaonekani tena.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nimeeleza kwamba mle mnamotokea malaria huwa ni kesi chache mno, nne, tano, tatu, mbili na huwa kwa kipindi hasa hiki kilikuwa ni kipindi cha mvua za vuli. Lakini kwa jumla bado Zanzibar malaria ni chini ya asilimia moja kitaifa kama vile tunavyoeleza UKIMWI. Wapo wagonjwa wa UKIMWI lakini bado Zanzibar nzina ni asilimia moja ya Wazanzibari ndio wanapata UKIMWI, lakini ukienda kwa makundi maalum UKIMWI unaongezeka. Kwa hivyo, na malaria ni hivyo hivyo, kwa jumla Zanzibar malaria tumefanikiwa ni chini ya asilimia moja. Kesi zinazotokea moja katika sababu ni usafi wa maeneo, zinaponyesha mvua maji yanakusanyika, madimbwi vile vimelea vinapata sababu ya kujitokeza na hilo huwa linashughulikiwa kila tunapopata taarifa tunalifuatilia.

Kuhusu kwenda kwenye Vituo vya Afya na watu kuambiwa hawana malaria. Waheshimiwa siku moja nilisema hapa mimi si mtaalamu, lakini moja katika kosa linalotokea katika jamii ni kuwa na homa ukasema nina malaria ukaanza kula dawa, unapokujakuwa sasa uende ukaangaliwe hayaonekani hilo moja.

Lakini pili unausababisha mwili wako kupunguza nguvu ya kukinga pale unapostahiki, si vizuri kama havikuonekana viluilui ukala dawa za malaria na ndio maana jana nilipokuwa ninajibu swali la *PHL* nikasema tuna tabia ya sample kuzichukua kwenye mahospitali tukazipeleka *PHL* kuthibitisha kwamba ni kweli wale wagonjwa waliopewa kesi ya malaria ni malaria kweli.

Kwa hivyo, naomba kuwaambia wananchi si vizuri kwamba huna hakika kuwa una malaria ukaanza kula madonge na kama unaambiwa kwamba basi chukua tu dawa ya malaria naomba uende mahali pengine pwenye uhakika ukaangalie kama una malaria ndio ule dawa za malaria, tunaifanya dawa iwe sugu na iwe haifanyi kazi kwa sababu ya kula dawa ovyo. Nilipokuwa Cuba nimeoneshwa athari ya jinsi maradhi ya malaria yalivyoathiri Afrika ya Magharibi kwa watu kula dawa bila ya mpangilio. *Prevalence* anayosema Mheshimiwa ni kwamba bado tunaendelea kusema kwamba sisi tuko chini ya asilimia moja na hizo kesi zinazotokea ni kesi maalum kwa mahali maalu na si kesi ambazo zinafanya kuonekana kwamba malaria yameongezeka kwa kiasi hicho.

Mhe. Spika: kulikuwa na sehemu ya swali lake kwamba zana hizi ziliopo zimepitwa na wakati ndio maana zikawa hazioneshi hivyo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, zana ziliopo ninazozifahamu mimi tunazotumia ni nzima, kuna watu wengine wanakwenda kupima malaria kwenye vituo vya binafsi. Hivyo siwezi kuthibitisha labda niwaambie watu wa Idara yangu ya Malaria nao kuvipitia kuviangalia. Lakini vile vya hospitali yetu vinafanywa kitaalamu wiki tatu au mwezi mmoja uliopita nimekwenda kuzindua lebo ya Mnazi Mmoja kwa taarifa yeno ni *one of the best in Africa,* lebo ya Mnazi Mmoja imekuwa *classified* hivyo. Kwa hivyo, ukienda Mnazi Mmoja kule juu ukiambiwa huna basi umefika mahali ambapo kuna utaalamu, lakini ile ya kwenda Mkunazini sina hakika Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu a, b na c.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada yao ya kupambana na malaria katika nchi yetu na *Inshaallah* kwa jitihada yao Mwenyezi Mungu atatusaidia.

(a) Mhe. Spika, napenda nimuulize kuwa, kwa sababu amesema kama malaria huwa yanazidi katika kipindi hiki cha mvua na kwa sababu sasa hivi tunaingia katika msimu wa masika. Je, wamejipanda vipi kutoa elimu zaidi kwa wananchi na hasa ukiangalia kuwa wananchi hawajui kuwa ukila dawa malaria haionekani, kwa hivyo kabla ya kwenda hospitali wasimewe dawa. Sasa amejipanga vipi kutoa elimu kwa wananchi kwa Zanzibar nzima ili kulijua suala hilo.

(b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu amesema kwamba sasa hivi dawa zinazotumika ni dawa mchanganyiko na dawa hizi Mhe. Spika, zina nguvu nyingi sana na kama umekula dawa hizi kama una malaria au homa tu ya kawaida basi inazidi zaidi na inabidi kama hukulazwa basi wende ukalazwe. Je, hakuna dawa nyengine mbadala ambayo inaweza kuwatibu wananchi na tukaachana na dawa hii ya mchanganyiko.

(c) Mhe. Spika, kwa sababu malaria..

Mhe. Spika: Hivi tunaruhusu maswali mangapi, nadhani hilo uliache.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunisaidia kwa kupunguza maswali kwa utaratibu. Swali la Mhe. Mjumbe ni kwamba tumejipangaje kwa kutoa taaluma. Tuna kitengo chetu maalum cha *Public Health Promotion* ambacho huwa kinafanya hivyo, kwa malaria inaonekana tumefanya juhudi kubwa sana. Kwa sababu kila siku namsikia Bi Kidude anavyotoa matangazo yake, hupiga yaleli moja nene pale halafu akawaambia watu tafadhalini jificheni kwenye vyandarua mlivyopewa msiviweke masandukuni. Hiyo ni moja katika mipango yetu ya kuendeleza taaluma hiyo na kwa nafasi hii basi wananchi mvua hizi zinazonyesha vimelea huwa vinapata nafasi kukusanyika. Kwa hivyo, tujitahidi kila penye maji yaliyokuwa hayana sababu aidha tuyafukie au tuyamwage kwenye videbe.

La pili suala la dawa. Dawa kama mnakumbuka kulikuwa na *chloroquine*, kukaja *materquine,* ma-*quine* yakawa mengi, zinafika hatua kwa huo mfumo wa watu kula dawa ovyo zinakuwa hazifanyi kazi tena. Kwa sasa wataalamu baada ya kufanya uchunguzi mchanganyiko wa dawa hizi ndio mchanganyiko ambao sasa unafanya tiba ya malaria itibike. Ni vizuri mwananchi kwa sababu dawa zina nguvu angalau basi upate japo uji au ugali kabla hujala na ni kweli mara nyengine tunakula dawa bila ya kula chakula na zinatusumbua. Kwa hivyo, Mheshimiwa kwa taarifa yako tutaendelea kuongeza kampeni kuwaelimisha wananchi wetu hasa wakati huu wa mvua na taarifa hii nadhani na Mkurugenzi wangu nitamfikishia ili tuongeze kampeni hiyo wakati huu na jinsi ya kula dawa za malaria. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tukubali kwamba swali limechukua muda mrefu waziri amejitahidi namshukuru. Tuendelee.

Nam. 89

Skuli ya Jeshi *Ali Khamis Camp*

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Ndugu zetu wanajeshi pale *Ali Khamis Camp,* Vitongoji wamejenga skuli kwa lengo la kuisaidia serikali, kuinua kiwango cha elimu Zanzibar. Lakini jambo la kusikitisha kwa skuli hiyo hawapati mashirikiano yoyote na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuwaunga mkono wanajeshi hao katika kusaidia maendeleo ya skuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Spika, na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 89. Kwanza, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa wanajeshi wa kikosi cha *Ali Khamis Camp* kilichopo Vitongoji Pemba wameanzisha skuli ya msingi ambayo inatumiwa na watoto wa wanajeshi na raia wanaoishi maeneo ya karibu na kambi hiyo.

Wizara yangu inalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa juhudi zao za kuanzisha skuli hiyo ambayo inawasaidia watoto wengi kupata elimu katika eneo la karibu ya sehemu wanayoishi.

Hata hivyo, sikubaliani na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba wamiliki wa skuli hiyo hawapati mashirikiano kutoka katika wizara yangu. Wizara imeshirikiana nao kikamilifu tokea hatua ya ujenzi wa skuli hiyo ambapo wizara yangu imechangia shilingi 9,000,000/- kwa kukupiga plasta, kutia sakafu na kupaka rangi. Pia, wizara yangu imetoa mwalimu mmoja ambaye anafundisha katika skuli hiyo. Hivyo si sahihi kwamba wizara yangu haiungi mkono maendeleo ya skuli hiyo kwani inafanya hivyo kwa kutambua umuhimu wa skuli hio kwa maendeleo ya watoto wetu bila ya kuangalia kuwa skuli hio inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kuna taarifa kuwa ndugu zetu hawa Wanajeshi wana nia ya kukabidhi skuli hii kuendeshwa na wizara. Je, suala hili ni kweli, kama ni kweli ni sababu zipi zinalizopelekea kucheleweshe mchakato huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa kuwa wamiliki wa skuli hiyo wana nia ya kuikabidhisha skuli hio katika Wizara ya Elimu. Mimi binafsi nilifanya ziara ya kwenda katika skuli ile badala ya mazungumzo yangu na Mwakilishi wa jimbo lile kunieleza matatizo yaliyopo katika skuli ile. Nilifanya ziara yangu mwezi wa Septemba mwaka jana na nikaonana na uongozi wa skuli tukakubaliana, lakini Mhe. Spika, kama ujuwavyo kuwa skuli ile ni skuli ya jeshi na jeshi wana taratibu zao. Mimi nilitaka wawasiliane na Makamo Makuu yao ili watuandikie barua rasmi kuwa skuli ile wanatukabidhisha halafu hatua nyengine zitaendelea, lakini mpaka sasa bado sijapata barua yoyote ya kutueleza kuwa tayari wamekubaliana na yale mambo tuliyokubaliana katika skuli ile.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza kabla ya kuuliza nachukua fursa hii kumpongeza Mkuu wa Majeshi Tanzania *CDF* pamoja na Uongozi wa Kambi ile ya *Alhamis Camp* kwa kuweza kutujengea skuli nzuri kama ile ambayo inatoa elimu ya viwango kwa kweli. Baada ya maelezo yaho Mhe. Spika, nauliza swali langu.

Kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wanafunzi walioko pale ni wanafunzi kutoka uraiani, yaani wazazi wao ni walipa kodi wa nchi hii, na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakiri kwamba tangu ianzishwe skuli ile kapelekwa mwalimu mmoja tu kutoka Wizara ya Elimu kwenda kufundisha pale na kwa kuwa skuli ile Wanajeshi wamejenga majengo mengi yaliyogharimu mamilioni ya mashilingi na kakiri kuwa Wizara ya Elimu imetoa shilingi milioni tisa tu, ambapo hata nusu jengo haliwezi kupatikana pale.

Je, kufanya hivyo si kurudisha nyuma maendeleo na kuwavunja moyo wanajeshi katika kuleta maendeleo nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyozungumza awali kuwa mimi mwenyewe binafsi nilikwenda katika skuli ile, skuli ile ni kweli ina wanafunzi wengi wa kiraia na jumla ya wanafunzi pale ni 502.

Lakini skuli ile Mhe. Spika, haina tatizo la walimu ina walimu 19 ambapo kati ya hao saba ni walimu waliosomea ualimu, wengine watatu ni *Form VI*, watatu wengine tumewachukua sisi wenyewe Wizara ya Elimu tumewapeleka *TC* kwa ajili ya kujiendeleza. Kwa hivyo, kupeleka mwalimu mmoja ni katika kuonesha yale mashirikiano tu, lakini kwa kweli katika skuli ile hakuna tatizo la walimu na walimu waliopo wanatosheleza kabisa katika kutoa taaluma katika skuli ile.

Nam. 159

Tatizo la Maji Pete

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Chama cha Mapinduzi kiliahidi katika Ilani ya Uchaguzi kuwapatia huduma ya maji safi wananchi wake Mjini na Vijijini.

(a) Je, serikali inatekeleza vipi ahadi hiyo kwa wananchi wa Pete ambao tatizo lao kubwa ni ukosefu wa maji.

(b) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu serikali ina mpango gani wa kumalizia kazi iliyobakia baada ya Mwakilishi wa Wananchi kufanikiwa kumalizia tatizo la *pump* ya maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsane Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 159 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa ufafanuzi juu ya hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba serikali kupitia wizara yangu inatekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya kuwapatia wananci wa Pete huduma ya maji safi na salama.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi hao huduma hiyo. Miongoni mwa juhudi hizo ni zile zilizofanywa za kubadilisha miundombinu ya mabomba ambayo yalikua yakivujisha na kwa sasa kilichojitokeza ni kupasuka kwa bomba na mafundi wetu wanaendelea na jitihada za kulifanyia ukarabati na pindi itakapomalizika kazi hiyo basi tatizo hilo litapungua ama litaondoka kabisa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri mimi nakuheshimu sana na nitaendelea kukuheshimu kutokana na urafiki wetu, nimestahamili mengi pamoja na suala la Kengeja la jana kuwa ile kazi haijafanyika mpaka sasa nikaridhia nayo. Wananchi wa Pete wamejaribu kugharamia shilingi milioni nane kwa jitihada zao wakanunua mpira kutoka Unguja Ukuu hadi karibu na Pete. Hicho kitu mafundi wako wanajua na wakafanya jitihada hayo maji yakafika baada ya mwezi mmoja yakakatika *pump* zimechanika kutokana na nguvu ya maji. Mara ya pili nilipokuuliza swali katika kikao kilichopita ukanambia maji hayo yatapatikana, nikaheshimu maamuzi yako, lakini kwa uchungu wale wananchi wanateseka na wanaumia.

Wizara yako nikakaanayo mimi pamoja na wananchi wangu wakaambiwa wachague mambo mawili kati ya hayo, ama kununua *pump* au mipira ya maji wakakubali kupeleka *pump.*

Mhe. Spika: Mheshimiwa uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa ukiangalia Jambiani, Jozani, Muungoni wanakosa maji kuna jitihada gani za kuwapelekea maji na wakati hivi sasa na Mfumbwi maji yake ni ya kipindi cha mvua na baada ya muda huenda wakapata maradhi ya kipindupindu Mwenyezi Mungu awanusuru kwa hilo. Je, kuna utaratibu gani wa kuwapelekea *pump* wananchi wa Jambiani na Pete.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, bado naomba nimjibu kutokana na hiki kijiji cha Pete ambako ndiko kwenye tatizo kubwa la maji kwa sasa hivi.

Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeliona tatizo hilo na kwa jitihada za kulifanyia ukarabati tatizo hilo, basi namhakikishia kwamba tatizo hili litakaa sawa si muda mrefu. Hivi sasa ninavyozungumza basi mafundi wangu wako katika Kijiji cha Pete kulirekebisha tatizo hilo.

Mhe. Spika: Kuna taarifa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, swali langu la pili kuhusu wananchi wa kijiji cha Mfumbwi hivi sasa maji yao yanahatarisha afya zao na pampu yao imeharibika. Je, Mhe. Waziri anatoa ahadi gani kuwapelekea pampu mpya kwa muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli kuna kasoro ndogo katika kijiji cha Jambiani Mfumbwi tatizo ambalo linasababishwa na pampu. Lakini hilo tayari tumeliona na hivi sasa tunajipanga kwenda kulifanyia marekebisho, asiwe na wasi wasi hilo suala tunalishughulikia.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika ahadi zake aliahidi kwamba kuna vijiji atavitembelea kama vile Jang'ombe, Mpendae ambapo vijiji hivyo sasa hivi vina ukosefu wa maji. Je, Mhe. Waziri ahadi ile uliitekeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli nimeahidi kwamba nitatembelea baadhi ya vijiji vyenye matatizo ya maji na hilo nimelifanya, lakini nimelifanya kwa vijiji

ambavyo wawakilishi wao wameshirikiana na mimi. Kama Mhe. Mwakilishi Asha Bakari Makame kanipa taarifa tukaondoka na yeye na tukatembelea katika eneo lake na tayari tumeshaligundua lile tatizo.

Kwa wale wawakilishi ambao hawajanipa taarifa au hawajaja kwangu tukashirikiana basi sijenda. Lakini ninachowaahidi kwamba watakaponipa taarifa kwamba wameshakuwa tayari twende tukaangalie basi mimi niko tayari na tutakwenda pamoja na *inshaallah* tutajitahidi kufanya kila linalowezekana ili tufanye marekebisho na wananchi hawa wa vijiji hivyo wafanikiwe katika huduma hiyo.

Nam. 96

Ufinyu wa Stendi ya Chake Chake

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Kutokana na ongezeko la magari kisiwani Pemba stendi ya magari iliyopo sokoni Chake Chake Pemba imeshazidiwa na kukosa uwezo wa kukusanya magari ya abiria na ya mizigo. Hali hii husababisha msongamano mkubwa wa magari na vyombo vyengine vya moto na pia kusababisha usumbufu kwa watu wanaotembea kwa miguu.

(a) Je, Wizara yako imeliona hilo.
(b) Je, Wizara ina mipango gani ya kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Nam. 96 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba soko la Chake Chake limezidiwa kutokana na mahitaji na ongezeko la matumizi sokoni hapo yanayotokana na maendeleo ya jamii yetu.

(b) Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina mpango wa kuongeza eneo kwa ajili ya kufungua mlango mwengine mmoja ambao utatumika kwa kuingilia na mwengine kwa ajili ya kutokea magari katika stendi ya Chake Chake. Mbali ya hivyo Wizara ya Miundombinu ikishirikiana na Baraza la Mji wa Chake Chake, Shirika la Umeme Zanzibar *(ZECO)*, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Idara ya Upimaji, pamoja na Shirika la Posta kwa ajili ya kushirikiana kuondoa miundombinu ambayo ingezuia utanuzi wa stendi hiyo. Mfano wa miundombinu hiyo ni viwanja, nyaya, nguzo za umeme, mabomba ya maji na vyenginevyo. Aidha, maeneo ya nyuma ya stendi hiyo tayari yameshapatiwa ufumbuzi na wafanyabiashara wadogo wadogo wameshaondoshwa na kupelekwa katika soko jengine liliopo maeneo ya Tibirinzi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na kukiri kwamba sehemu ile ya stendi ya Chake Chake imezidiwa na wana mpango wa kutoa barabara nyengine ya kutoa magari baada ya barabara hii ambayo inaingia magari na kutoka kwa barabara hiyo hiyo moja. Je, suala hili litatekelezwa muda gani ili kuondoa msongamano huu ambao hivi sasa upo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, jukumu la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika soko lile la Chake Chake ni kuratibu na kuona kwamba magari sehemu ya kusimamia yanapatiwa ufumbuzi ili kuondoa msongamano uliopo.

Mhe. Spika, tatizo liliopo ni kwamba eneo linalotumika hivi sasa kwa ajili ya kuegesha magari pamoja na kuzungusha limekuwa dogo. Kikwazo kinachosababisha eneo hilo kushindwa kutengeneza barabara ya pili kilikuwa ni miundombinu ya nyaya, nguzo, pamoja na nyumba. Takriban shilingi milioni 39,760 zimetengwa kwa ajili ya kufanikisha suala hilo.

Aidha, ni imani yangu kwamba tutakapoweza kupata ufumbuzi wa nyumba moja iliyosalia kwa sababu tayari wafanyabiashara wameshaondoshwa viwanja vile ambavyo vilikuwa vimetolewa na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi vimeshafutwa na kupatiwa viwanja vyengine. Ni imani yangu kwamba mazungumzo yanaendelea ya kuihamisha nyumba iliyopo hivi sasa basi jambo hili litapatiwa ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Kwa muda huu hatutoweza kusema lini tutalipatia ufumbuzi suala hili hadi pale mazungumzo ambayo tumeanza

na mmiliki wa nyumba atakapokubali kuhama katika nyumba yake na kukubali kuivunja ili sasa ujenzi huu tulioutarajia uweze kuendelea.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kama Mhe. Naibu Waziri alivyosema kwamba tatizo ni kukosa stendi pamoja na *road network.* Ni kweli kwamba tatizo kubwa linaloisumbua Chake Chake hivi sasa ni kukosa stendi pamoja na *road network* ya barabara katika mji wetu.

Nakumbuka kwamba Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilikuwa na mpango wa kuweka stendi mpya katika bonde la Michakaeni. Je, Mhe. Waziri mpango ule wa kulifukia bonde la Michakaeni umefikia hatua gani.

Lakini swali (b) kama laitani serikali ingeliimarisha njia ndogo ndogo zilizomo katika mji kama vile Mkokotangozi kwenda Soko la Samaki, njia ya Msingini, njia ya Mwanamashungi/*ZSTC*, pamoja na njia ya Mapinduzi/Mgogoni, basi kwa kiasi kikubwa ingeliondosha tatizo la msongamano wa magari pamoja na *parking* katika mji wa Chake Chake. Je, Mhe. Waziri katika bajeti ya mwaka 2012/2013 serikali imetenga kiasi gani katika kulitatua tatizo hili.

Mhe. NaibuWaziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, swali la kwanza alilouliza Mhe. Mwakilishi amekiri na kusema wazi kwamba hii ni mipango ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama Wizara inayoshughulika na usimamizi wa Mipango Miji kwa kupitia Halmashauri na Manispaa. Hivyo basi, ni imani yangu kwamba serikali itakuwa imelisikia na tutawasiliana na wizara husika ili kupatiwa majibu kwa maandishi na tutamletea Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, swali la pili anauliza kuhusiana na barabara ndogo ndogo. Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuliarifu Baraza lako tukufu wajibu wa wizara yetu na ushirikiano tuliokuwa nao wizara yetu pamoja na halmashauri na manispaa zinazoongoza miji yetu ya Zanzibar. Wajibu wa wizara yetu ni barabara kubwa na barabara hizi ndogo ndogo ni wajibu wa halmashauri na manispaa.

Lakini pia kwa kushirikiana na halmashauri hizo pamoja na manispaa na kwa kupitia fedha za Mfuko wa Barabara tutaendelea kuzifanyia matengenezo na kujenga barabara mpya kila pale hali inaporuhusu. Lakini kwa kusema moja kwa moja katika bajeti yetu mpaka muda huu bado jambo hili hatujaliingiza kwa sababu liko katika taasisi nyengine zinazohusiana na Mfuko wa Barabara.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba vikwazo ni nguzo za umeme, nyaya na mambo mengine. Lakini kwa sababu suala hili mimi nalijua na kamati yetu imelishughulikia suala hili ikiwa nao ni mdau mkubwa wa suala hili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama kikwazo kikubwa ni jengo ambalo ni nyumba na inasemekana nyumba hii kwanza ilikuwa ni ya Mama Fatma Karume ndie aliyeinunua na baadae kamuuzia mtu mwengine. Nyumba hiyo inataka kulipiwa sijui shilingi milioni 100 na zaidi.

(a) Je, serikali itakuwa tayari kulikabili jengo hili ili liondoke kwa ajili ya kufunguliwa njia nyengine gari zinazoingia ziwe zinatoka sehemu nyengine.

(b) Je, atakubaliana na mimi kama ikifunguliwa njia hiyo pale sehemu pamoja na udogo wake lakini itakuwa inaondoa msongamano wa magari na watu watakuwa wanaingia na kutoka bila shida yoyote. Ni lini sasa wizara au serikali itakuwa tayari kulishughulikia suala hilo la jengo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza kwamba stendi ya Chake Chake ina matatizo na matatizo haya yanatokana na ufinyu wa eneo lenyewe. Vile vile tumeeleza changamoto au vikwazo vinavyotusababisha kuzuia utanuzi wa stendi ile kwamba ni miundombinu zilikuwepo nyaya, mipira ya maji, nguzo za umeme, lakini pia kulikuwa kuna viwanja vya watu ambavyo vilikuwa vimegaiwa kwa ajili ya ujenzi wizara husika imevifuta. Tumeeleza pia kwamba kuna nyumba ambayo bado idara husika inaendelea na mazungumzo, ni imani yetu kwamba idara husika itafika pahala itakubaliana na mwenye nyumba, watakubaliana kulipa fidia nyumba itaondoshwa na utaratibu wa kuiendeleza stendi ile utafikiwa.

Mategemeo yangu kwamba hakuna mwananchi wa Zanzibar atakayeombwa na serikali kwa msingi wa kuendeleza maendeleo ya nchi yetu na yeye yuko tayari kufidiwa gharama zake akakataa nia na malengo yale ya

serikali kwa manufaa yake binafsi kuzuia maslahi ya wengi. Mategemeo yangu kwamba mwananchi yule nae ni mwelewa, ana uchungu wa nchi hii atafahamu malengo ya serikali na atakubali fidia ile ili apishe utanuzi wa stendi hiyo.

Jibu (b) mategemeo ya wizara yetu kwamba ile nyumba ikiondoka tukiweza kuongeza *network* ya barabara basi ule usumbufu wa magari utakwisha kabisa katika stendi ya mji wa Chake Chake.

Nam. 44

Hali ya Kiwanja cha Ndege Pemba

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Kwa kweli hali ya Kiwanja cha Ndege Pemba inasikitisha. Ni lini Wizara itakuwa tayari kuanza matengenezo na ushughulikiaji kwa ujumla wa kiwanja hicho.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kipindi kirefu Kiwanja cha Ndege Pemba hakipo katika hali nzuri ya kuridhisha kwa ajili ya kutoa huduma usiku na mchana. Hali hiyo inatokanana upungufu wa baadhi ya vifaa vya vitendea kazi. Lakini Wizara yangu katika juhudi za kufanya kiwanja hichi kuweza kukidhi na kuwa cha kisasa serikali kwa kupitia wizara husika chini ya usimamizi wa Viwanja vya Ndege Zanzibar juhudi zifuatazo zimechukuliwa.

(a) Wataalam kutoka South Africa chini ya usimamizi wa Kampuni ya *ADB, Airfill Dissolution* na *Safe Gate Company* zote za Afrika Kusini tayari wameshafanya utafiti wa juu ya uwekaji wa taa za njia ya kutulia na kurukia kwa ndege *(runway)* na tunasubiri taarifa yao ili tuendelee na hatua ya utekelezaji wake. Hatua hii itakifanya kiwanja chetu cha Pemba kuweza kutoa huduma za kutua na kuruka kwa ndege kwa wakati wote.

(b) Mhe. Spika, katika hatua nyengine tayari hatua ya kutafuta *standby generator* lenye uwezo wa 250 KVA nazo zinaendelea na matumaini yetu si muda mrefu *generator* hili litapatikana ili kuweza kutoa huduma za umeme muda wote katika uwanja ule. Mategemeo yetu kwamba makisio haya yatafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Aidha, wizara katika hilo pia kuna mpango wa muda mrefu wa kukiimarisha kiwanja chetu kilichopo Pemba ikiwa ni pamoja na kuongeza urefu wa njia ya kurukia na kutulia kwa ndege kutoka mita 1,550 hadi 1,850. Pia tuna mpango wa kujenga jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege Pemba.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri na ya kutia moyo ya Mhe. Naibu Waziri na naomba labda niseme kwamba hizo hatua ziwe za kweli lakini naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri katika maelezo yake yote hakugusia kuhusu jengo lililopo sasa hivi na ndilo linalotumika na jengo lile linavuja. Je, kuna mpango gani wa dharura ambao utachukuliwa ili mvua hizi za masika angalau ile *VIP* Rais akenda asije akavujiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza napenda kumtoa hofu Mhe. Mwakilishi kwamba kauli tunazosema hapa ni kauli za kweli na tunazisema kwa nia ya dhati kabisa. Sisi ni Wazanzibari na tuna uchungu kuona nchi yetu inapiga hatua za kimaendeleo.

Mhe. Spika, ni kweli maelezo aliyoyatoa Mhe. Mwakilishi kwamba jengo letu la Pemba sasa hivi lina matatizo. Lakini sisi kama Wizara tuna usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Zanzibar tayari tumeshachukua hatua ikiwa ni pamoja na kutafuta mafundi kufanya makisio. Takriban shilingi milioni 275 zinahitajika ili kuweza kufanya uezekaji pamoja na matengenezo mengine muhimu kwa jengo lile. Mategemeo yetu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Serikali Kuu tutapata fedha hizi haraka iwezekanavyo ili kunusuru hiyo hali anayoeleza Mhe. Mwakilishi.

Nam. 51

Mnara wa Matangazo

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni mnara wa matangazo Chumbuni umeondolewa na eneo la kituo hicho limezungushwa uzio tofauti na ilivyokuwa zamani.

(a) Je, mnara na kituo hicho cha kurushia matangazo kimehamishiwa wapi.
(b) Mnara na Kituo cha Chumbuni kilikuwa kinarusha matangazo ya masafa gani.
(c) Kwa vile eneo hilo limezungushwa uzio. Je, ni nani aliyeweka uzio huo na kwa sasa liko chini ya umiliki wa taasisi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mnara wa kituo cha kurushia matangazo ya redio kilichokuwa Chumbuni Wilaya ya Mjini sasa umehamishiwa Bungi Wilaya ya Kati Unguja.
(b) Kituo cha redio cha kurushia matangazo kilichokuwa Chumbuni kinarusha matangazo ya masafa ya kati *(medium wave).*
(c) Eneo la Chumbuni limezungushwa uzio na serikali kwa kutumia Idara ya Ujenzi na hadi hivi sasa katika eneo hilo viko vifaa vya utangazaji ambavyo vitahamishiwa huko Bungi lakini bado hadi hivi sasa serikali haijaamua eneo hilo litumiwe na taasisi gani.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini redio mara nyingi inakwenda sambamba na mawasiliano ya simu. Sasa katika eneo la Kikwajuni kuna mnara wa *Wireless* ambao kwa sasa haufanyi kazi na hauna taa juu unasababisha hatari. Je, Wizara yako ina mpango gani katika kusaidia suala la mnara ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kusaidiana na Naibu Waziri mwenzangu katika kutoa ufafanuzi wa swali lililoulizwa.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika maeneo ya *Wireless* kulikuwa kuna mnara na mnara ule ni miongoni mwa minara mikongwe iliyojengwa katika Afrika Mashariki na ulikuwa ukitumika wakati huo kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali. Lakini kwa kipindi hiki maamuzi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuuondoa mnara ule kutokana na uchakavu wake na huenda ukasababisha athari kubwa pindi ukianguka pengine ukapelekea majanga kwa wananchi wetu. Maamuzi ya serikali ni kuuondoa mnara ule na kujenga mnara mwengine utakaoweza kukidhi mahitaji ya simu.

Lakini pia Mhe. Spika, tusisahau kwamba dunia sasa hivi inabadilika na tunakwenda kwenye mfumo wa *digital* matumizi ya minara pengine hayatokuwa kwa muda mrefu kama ulivyokuwa ule ambao umeishi zaidi ya miaka 100. Mategemeo yetu sasa hivi minara haitokuwa na uwezo wa kuishi zaidi ya miaka 25 kwani sayansi imebadilika katika eneo hilo la mawasiliano.

Hoja za Serikali

Ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe binafsi kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii. Lakini la pili naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe ambao nadhani karibu 9 walichangia katika hoja hii jana. Mhe. Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe ambayo ilitolewa jana jambo moja lilikuwa la dhahiri kabisa kwamba kutokana na hoja hii iliyotolewa na taarifa iliyoletwa kuwa kuna

mambo ambayo yana upungufu. Upungufu wenyewe ni kwamba taarifa ambayo imeletwa imezingatia zaidi marekebisho baada ya lile tatizo, lakini kile kiini cha tatizo lenyewe ni wazi na nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kwamba kwa hakika halikuelezwa hasa lile tatizo ambalo Waheshimiwa Wajumbe walilieleza katika kikao kilichopita na ambalo walitaka lifanyiwe kazi.

Sasa kwa sababu hiyo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 54 ya kufanya marekebisho katika hoja iliyoletwa ya serikali kwa kuongeza kwamba badala ya ile ripoti iliyoletwa na serikali basi tuongeze nyongeza ya taarifa ya ripoti ya Kamati ya Kazi Maalum ya Baraza la Manispaa ambayo iliundwa tarehe 5 Mei, 2011 taarifa ambayo imegaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba iwe ni sehemu ya hoja hii ya serikali na ili wajumbe wapate fursa ya kuijadili nayo na baadae kuja kutoa uamuzi nini cha kufanya pia kupata fursa ya kuijadili na kuitolea maoni hii taarifa ya kamati ambayo nimeitaja na ambayo imeshagaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwa sababu ya mabadiliko hayo ambayo nayapendekeza katika hoja hii naomba pia kutoa hoja chini ya kanuni ya 63 kwamba mjadala basi wa hoja hii uahirishwe ili kuwapa fursa Waheshimiwa Wajumbe waipitie ripoti hii ya kamati ambayo nimeitaja. Baadae Mhe. Spika, siku ambayo utaipangia ya kuja kujadiliwa tena hoja hii tuendelee kuja kuijadili na tupate fursa ya kutoa maamuzi na ili kuleta ufanisi na kupata fursa ya kuweza kuijadili vizuri. Siku hiyo tunaomba kwamba iwe katika mkutano huu wa Baraza. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Naona Waheshimiwa Wajumbe mmeifanya kazi yangu iwe nyepesi sana, maana haya makofi yaliyoingia yanamaanisha kwamba Waheshimiwa Wajumbe tunakubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu na ukizingatia kanuni hiyo ya 54 basi kwa kweli Spika ndiye ambaye anapaswa aseme kwamba ni sawa au sio sawa. Mara nyingi huwa sipendelei kusema moja kwa moja bila ya kuona dalili za wajumbe wangu wanasemaje na hapa nimeiona kwamba dalili inakubalika.

Labda niseme jambo moja tu nikitilia mkazo na maana kubwa ya hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwanza kabisa Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwamba michango yetu tunayotoa katika Baraza hili inakuwa ya wazi na pale ninapoomba tuwe tuna mkutano mmoja tu huwa napenda sana sote tusikie mjumbe/wajumbe wenzetu wanavyoeleza na inasaidia kupata maoni, mashauri mbali mbali ambayo yanatolewa katika Baraza hili.

Ni kweli kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu katika hoja yake kwamba jana yalitoka maoni mbali mbali juu ya ripoti iliyowasilishwa kwa njia ya hoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba ripoti iliyokuja haikuwaridhisha Waheshimiwa Wajumbe na yakatoka mashauri.

Nakumbuka Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni mmoja aliyeshauri kwamba tena ilianza kwa Mhe. Omar Ali Shehe kwamba kuna ripoti ambayo hiyo ndio iliyofafanua hasa hayo mambo ambayo yanahusika ikaungwa mkono na Waheshimiwa Wajumbe wengi na kwa usikivu wa serikali wakaona hilo jambo walizingatie wakanitumia taarifa tangu jana kwamba wanayo nia ya kufanya mabadiliko haya na nikaelekeza sawa tuje tuone tunafanyaje.

Nashukuru kwamba Waheshimiwa Wajumbe jambo hili lina umuhimu, na kwa kuzingatia yale maelezo mengi ambayo niliyoyatoa jana, basi umuhimu wa kubadilisha hoja hii inakubalika na mimi nakubali chini ya kifungu hicho cha ibara ya 54 ya kanuni zetu, kwamba hoja hii ibadilishwe.

Kwa maelekezo ya kusambaza ripoti ile nyengine, kwa sababu itakuwa ni ripoti mpya na ina mambo mengi kidogo. Hata Mhe. Waziri alisema kwamba ripoti hiyo ilikuwa ni kubwa, kwa hivyo itahitaji muda Waheshimiwa Wajumbe waingie ndani, ili baadae tuje tuijadili.

Sitaki leo na wakati huu niseme itakuwa lini, tutaangalia mpangilio wa shughuli zetu, lakini ilimradi shughuli hii tunategemea sana inaweza ikashughulikiwa wiki ijayo.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, nakubali kusitisha mjadala huu na kubadilisha hoja hiyo, ili wiki ijayo sasa tuweze kuijadili tukiwa pamoja na zile ripoti nyengine ambazo nategemea wanaohusika watakuwa wanaisambaza na Waheshimiwa Wajumbe mpate kuipitia ili wiki ijayo tuweze kwenda vizuri zaidi.

Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa maoni mazuri na ushauri mzuri. Pia niwashukuru serikali kwa usikivu, maana hili jambo nalo ni muhimu sana. Shughuli zetu zitakwenda vizuri zaidi tukiwa na uwiano wa aina hii. Wajumbe wanasema, serikali inasikiliza na hatimae tunafikia pahala kuweza kufanya kitu ambacho kitatupeleka mbele katika shughuli zetu kwa niaba ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, nakubali kuakhirisha mjadala huu hadi hapo wiki ijayo, wakati muafaka ambapo ripoti hii mpya inagaiwa kuanzia sasa hivi, Waheshimiwa Wajumbe mkaisome ili tuijadili wiki ijayo, nawashukuru sana. Ahsanteni tunaendelea. Katibu tunaendelea na shughuli inayofuata.

Hoja Binafsi Kuhusu Kuunda Kamati Teule Kuchunguza
Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) Dhidi ya Madai ya Kuwepo
Ukiukwaji Mkubwa wa Majukumu yake

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na uzima na nikushukuru wewe binafsi kwa mara ya mwanzo leo kunipa nafasi ya kusimama katika *membari* hii. Nilikuwa najiuliza *membari* hii nitaigusa lini. Lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu leo umeniruhusu, nakupongeza sana na ninakushukuru.

Mhe. Spika, kabla ya kuisoma hoja yangu naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, juu ya katiba ya Zanzibar kifungu cha 9(1). Kifungu hiki kinasema;

Kifungu cha 9(1)

"Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii"

Kifungu cha 9(2)

"Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe, na ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba hii kutatokana kwa wananchi wenyewe".

Mhe. Spika, pia niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, katiba hii kifungu cha 21 kinasema kama ifuatavyo.

"Kila Mzanzibari anayo haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi, ama moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa hiyari".

Mhe. Spika, baada ya kusoma katiba hiyo, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba nimebahatika kuwa na *file* zima ambalo nimetumwa na wananchi nije nilifanyie kazi kwa ajili ya shughuli hii, na sio matakwa yangu bali ni wananchi wa Zanzibar na wala sio wananchi wa Jimbo la Kiwani tu, ni majimbo yote ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya hapo sasa naomba uniruhusu niisome hoja yangu binafsi kama nilivyokuomba hapo kabla.

Mhe. Spika, hoja binafsi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuliomba Baraza la Wawakilishi kuunda kamati teule ya kuchunguza Shirika la Umeme la Zanzibar dhidi ya madai ya kuwepo ukiukwaji mkubwa wa majukumu yake.

Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar ni nchi inayoongozwa kwa misingi ya katiba na sheria na kwamba katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu cha 10(a) kinaeleza wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutoa huduma kwa watu wote na kutoa haki zote za kuishi wakiwa Zanzibar, sehemu zote za Zanzibar na kwamba maana ya serikali pia inajumuisha mashirika yote ya serikali, ikiwa ni pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa kuwa Shirika la Umeme Zanzibar, ni shirika la serikali lililoanzishwa kwa mujibu wa sheria nambari 3 ya mwaka 2006 na kwa madhumuni makubwa ya kutoa huduma ya umeme kwa watu wote wa Zanzibar, na kwamba sheria hiyo iliipa shirika majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na huduma ya nishati ya umeme Zanzibar. Kwa kuwa katika utoaji wa huduma Shirika la Umeme linahusika na usambazaji wa huduma ya umeme, ikiwa ni pamoja na kusimamia uungwaji wa umeme kwa wananchi wote wa Zanzibar na linapaswa kuhakikisha kwamba linatoa huduma hiyo kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa katika katiba ya Zanzibar na sheria.

Mhe. Spika, kwa kuwa ni jukumu la serikali kuhakikisha kwamba watumishi wake wote wanapinga vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa madaraka, na kwamba kwa muda wote kumekuwa na malalamiko ya wananchi, kwamba baadhi ya watendaji wa Shirika la Umeme hawana uaminifu katika kutoa huduma za uungwaji wa umeme kwa baadhi ya wananchi na kwamba hali hii pamoja na mambo mengine, inadhorotesha uwezo wa shirika kumudu dhima zake ikiwa ni pamoja na mzigo mkubwa wa deni linalodaiwa na *TANESCO*.

Mhe. Spika, kifungu cha 32 cha sheria nambari 3 ya mwaka 2006 kinaeleza wajibu wa mwananchi. Mteja anayetaka kuungiwa huduma ya umeme anatakiwa atoe ama anunue mita, *cut-out*, nguzo na vifaa vyote

vinavyohitajika kwa ajili ya kuungiwa na kupatiwa umeme, na kwamba wananchi wetu wanatekeleza matakwa hayo ya sheria huku wakitarajiwa kupatiwa huduma hiyo kwa muda muafaka na bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna malalamiko makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwamba wanapata usumbufu mkubwa wa kuungiwa umeme na Shirika la Umeme, huku wakishuhudia huduma hiyo ikitolewa kwa baadhi ya wamiliki wa hoteli, kampuni za minara ya simu za mikononi na benki bila ya usumbufu wowote na kwa haraka iwezekanavyo. Licha ya kulipia huduma za uungwaji wa huduma hiyo, bado wananchi hao wanapata usumbufu mkubwa wa kusubiri huduma hiyo wakati wanapoomba, ikiwa ni pamoja na kulipia bei kubwa wanapopewa, huku baadhi ya kampuni hizo zikilipia fedha ndogo zinazoingia katika mapato ya shirika.

Mhe. Spika, kwa kuwa huduma ya umeme ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi, wateja wengi huwa hawana budi kulipia ili waweze kuungiwa huduma hii. Lakini katika hali ya kusikitisha, fedha hizo zimekuwa haziingii katika mapato ya shirika kutokana na uungwaji holela wa umeme na kupelekea shirika kukabiliwa na hali ngumu ya kifedha, huku fedha nyingi zinazolipwa na kampuni na baadhi ya wananchi zinaingia katika mikono ya baadhi ya wafanyakazi wa shirika wasio waaminifu.

Kwa kuwa malalamiko haya ya wananchi walio wengi, yanaonesha wazi kwamba Shirika la Umeme kama yalivyo mashirika mengine ya umma, kwa kutumia mamlaka ya uajiri waliyopewa na sheria nambari 3 ya mwaka 2006, wanalalamikiwa kutumia vibaya fursa hiyo, kwa kutofuata ipasavyo taratibu za uajiri kisheria na badala yake zinadaiwa kufanya upendeleo au ubaguzi wa uajiri kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa kuwa malalamiko haya ya wananchi, pia yanaonesha wazi kwamba kuna baadhi ya waajiriwa wafanyakazi wa shirika hawana uaminifu, na kwamba wanajiuzia mali za shirika bila ya kufuata taratibu za sheria ya fedha ya mwaka 2005 na kanuni zake, na bila ya kufuata taratibu za sheria ya manunuzi na ugavi kwa mali za serikali na kanuni zake ya mwaka 2005, na kwamba hali hii inaligharimu sana shirika na serikali kwa ujumla.

Kwa kuwa kuna malalamiko ya wananchi kwamba Shirika la Umeme limekuwa likiingia katika mikataba mingi isiyo na tija kwa wananchi, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa majenereta 32 yaliyonunuliwa baada ya nchi yetu kuingia katika tatizo la ukosefu wa umeme, uliodumu kwa muda wa miezi 3 mnamo mwaka 2009.Lakini Shirika limeshindwa kuyaendesha majenereta hayo, kwa sababu ya gharama za mafuta wakati walipaswa kuangalia na kufahamu suala hili kabla ya kuyanunua, matokeo yake ni kupoteza fedha nyingi za wananchi bila ya tija yoyote. Wakati huo huo shirika lina deni kubwa inalodaiwa na *TANESCO*, kunakosababishwa na shirika kulimbikiza deni kwa muda mrefu bila ya uwezo wa kulipia.

Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ndio chombo cha wananchi na lina dhima ya kusimamia serikali pamoja na mashirika yake na kuhakikisha kwamba, watendaji wa serikali wanafahamu kwamba vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma, na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi.

Kwa hivyo, basi kwa kutumia kanuni ya 27(1) (m), 27(3), 48(1) na 49(1) za kanuni za Baraza la Wawakilishi, mimi Hija Hassan Hija, naomba kutoa hoja kuwa Baraza lako tukufu liridhie kuundwa kwa kamati teule kwa mujibu wa kanuni ya 117 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2011 ili kuchunguza Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kwa kuangalia maeneo yafuatayo.

1. Upotevu wa fedha za shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasio waaminifu.
2. Sababu za usumbufu wanaoupata wananchi wakati wa kuomba na baada ya kulipia huduma ya kulipia umeme, pamoja na suala la bei kubwa wanazopewa ukilinganisha na baadhi ya watu, kampuni, hoteli, benki na kampuni za minara ya simu za mikononi.
3. Taratibu za ajira katika shirika zinazodaiwa kuwa ni za upendeleo kwa Unguja na Pemba.
4. Iwapo mali za shirika zinauzwa kwa kufuata taratibu za sheria ya uuzwaji na ugavi wa mali za serikali na sheria nyenginezo zinazohusika.
5. Iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo Mtoni kulifuata sheria zinazohusika na kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.
6. Kiwango cha deni inayodaiwa Zanzibar na *TANESCO*, na iwapo kuna sababu za msingi za kuendelea kuwepo kwa deni hilo na athari zake kwa maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja.

(Hoja Ilitolewa Ijadiliwe)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Lakini pili nimpongeze sana Mhe. Hija Hassan Hija kwa kuleta hoja hii binafsi, ambayo madhumuni yake makubwa ni kupambana na ubadhirifu katika mali za umaa.

Mhe. Spika, napenda nilihakikishie Baraza lako hili tukufu kwamba serikali yetu ya Awamu ya Saba moja katika dhamira yake kubwa ni kupambana na ubadhirifu ndani ya vyombo vya umma. Tunaunga mkono sana jitihada zinazofanywa na wajumbe wetu, katika kufanya tathmini ya kutafuta kila njia ya kuzuia ubadhirifu huo.

Mhe. Spika, kwa kuwa hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija imeeleza kwa kina kuhusu upotevu wa pesa za serikali na mali za serikali. Mhe. Spika, naomba nipendekeze kwa Baraza lako hili tukufu na kumuomba Mhe. Hija Hassan Hija kwamba badala ya kuunda kamati teule, basi kwa kuwa kamati yetu ya PAC ina utaalamu mkubwa sana wa kufanya kazi hizi za kutizama upotevu wa fedha za serikali, pamoja na mali za serikali. Hivyo naliomba Baraza lako likubali kwamba Kamati ya PAC ndio ifanye kazi hii, ikimjumuisha na Mhe. Hija Hassan ambaye ana habari nyingi. Naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, wajumbe wa Baraza hili ni wasikivu na wapo kwa ajili ya kuwatetea Wazanzibari. Mimi binafsi kama mtoa hoja naiamini Kamati ya PAC, lakini zaidi naiamini serikali kwa sababu imekubali kwamba kuna haja kuchunguzwa kuwasaidia. Kwa msingi huo Mhe. Spika, naunga mkono hoja ya waziri, ahsante sana.*(Makofi).*

Mhe. Spika: Nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamis na leo ni Alhamis, mambo yanakuwa mepesi na safi. Kwa pamoja tunakubaliana kwamba shughuli hii ya kuchunguza kadhia hiyo ya Shirika la Umeme, kama ilivyoelezwa katika hoja ya Mhe. Hija Hassan ifanywe na kamati ya PAC. Wakati huo huo Mhe. Hija Hassan awemo katika shughuli hiyo.

Mhe. Hija Hassan Hija kuwemo kwake katika kamati hiyo, itasaidia sana maana ameonesha *file* moja kubwa sana. Siku niliyomwita ili anithibitishie ukweli wa jambo hili, basi alikuja na *file*hilo na nikamwambia sasa ninakubali kwamba jambo hili lije Barazani, ili tuone tunafika wapi. Kwa hivyo, Mhe. Hija Hassan atakuwa ni mtu muhimu sana kuongoza njia kwa kupitia kwa Mwenyekiti wa Kamati ya PAC ambaye atafanya kazi hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, ni kawaida kamati zangu zinapopewa kazi hua zinapokea na hii naamini imepokewa na itafanywa kwa ufanisi mkubwa. Kazi hii ifanywe na PAC kwa mashirikiano na Mhe. Hija Hassan mtoa hoja.

Hivi kuhusu utaratibu baada ya makofi ya maamuzi, hapana.Sio utaratibu, huo sio utaratibu kwamba baada ya maamuzi ya Baraza sasa kuhusu utaratibu.Ukae. *(Makofi/Vicheko).*

Ndg. Katibu wa Baraza: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa taarifa kuwa hapa ndio mwisho wa shughuli zilizopangwa katika Kikao cha Kumi, cha Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane la Wawakilishi. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa.

Mhe. Spika: Kwa siku ya leo. Kikao cha mwisho kwa siku ya leo lakini.

Katibu wa Baraza: Mwisho wa Kikao cha Kumi kwa siku ya leo Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na mawaziri, kwa mashirikiano makubwa sana mnayokipa kiti, ili kuendesha shughuli zetu hizi kwa ufanisi mkubwa.

Tunaelewa kwamba tuna kazi moja ambayo leo ilipangwa tuwe na semina kidogo ya kutuelekeza baadhi ya mabadiliko ya marekebisho ya kanuni yetu hii tunayoitumia. Kwa hivyo, nadhani muda huu utakuwa unatosha ili mara baada ya kuakhirisha shughuli yetu hii, sina hakika itakuwa na ukubwa gani semina hii, mimi nadhani tuje kesho moja kwa moja baada ya semina hiyo, ili Waheshimiwa Wajumbe wapate kwenda kuzidi kuzingatia yale tutakayopeana katika semina.

Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kusitisha shughuli zetu kuanzia sasa na kuakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 13/04/2012 saa 3:00 za asubuhi. Lakini mara tukitoka hapa tunapanda pale juu kwa ajili ya semina yetu. Ahsanteni sana.

(Saa 4:48 asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 13/04/2012 saa 3:00 asubuhi)